

Swali: Mchuuzi maana yake nini kama tunavyosoma katika *Hosea 12:7?*
na je tunaruhusiwa kuwa wachuuzi?

Jibu: Turejee.

Hosea 12: 7 “Ni MCHUUZI, mizani ya udanganyifu i mkononi mwake; anapenda kudhulumu”

Mchuuzi ni mtu anayefanya biashara ya kununua bidhaa na kuzisafirisha kwenda kuziua mahali pengine hususani nje ya nchi yake.

Utalisoma neno hili tena katika kitabu cha ***Wimbo ulio bora 3:6, Ezeieli 27:3, Ezeieli 27:20-22 na Isaya 23:8.***

Swali ni je biblia inaturuhusu wakristo kuwa Wachuuzi (yaani biashara ya kutoka nchi moja kwenda nyingine)?

Jibu ni ndio inaruhusu!, isipokuwa katika biashara yoyote ile ni muhimu kuzingatia viwango vya utakatifu na ukamilifu, Uchuuzi wowote

ukihusisha rushwa au biashara haramu ni kosa kibiblia, na pia ni hatari kama maandiko yanavyosema katika *Ezekieli 28:18*.

Ezekieli 28:18 “Kwa wingi wa maovu yako, KATIKA UOVU WA UCHUUZI WAKO, umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao.

19 Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele”

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

Mchuuzi ni nani? (Hosea 12:7).

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 13 (Kitabu cha Hosea).

Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).

**Je! Karamu za 'Idi' ndio zipo hizo tunazosisoma katika Hosea
(12:9)**

Je ni halali kwa mkristo kufanya biashara ya Forex?

Kalafati ni nini? (Ezekieli 27:9)

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp